

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 40 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JUNI 2024

KATIBU WA TSC AFANYA MKUTANO NA WATUMISHI NCHI NZIMA KWA NJIA YA MTANDAO

✓ **Asisitiza Watumishi kuzingatia Sheria,
Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma**



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza Mkutano uliohusisha watumishi wote wa TSC nchi nzima kwa njia ya Mtandao kilichofanyika tarehe 23 Mei, 2024.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

KONGOLE PROF. MURUKE KWA KUTEULIWA KUWA MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Tarehe 15 Mei, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Prof. Masoud Hadi Muruke kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Prof. Muruke amechukua nafasi ya Prof. Willy Lazaro Komba ambaye muda wake umemalizika. Katika kipindi chake cha miaka mitatu, Prof. Komba amefanya kazi kubwa na kuifanya TSC kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu.

Kuteuliwa na Rais kuongoza chombo hiki muhimu kinachosimamia Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu nchini sio tu kwamba ni jambo la heshima bali pia inaonesha

Prof. Muruke ni mtu muadilifu, mchapakazi mzalendo na mtu wa kuaminika.

Tume ya Utumishi wa Walimu imeahidi kutoa ushirikiano kwa Prof. Muruke ili aweze kutekeleza majukumu yake vizuri na hivyo kuiwezesha TSC kuendelea kuwa chombo Madhubuti katika kuendeleza Sekta ya Elimu kwa kuhakikisha Utumishi wa Walimu unasimamiwa ipasavyo.

Hongera Prof. Muruke kwa kuaminiwa na kuteuliwa, tuna imani chini ya uongozi wako huduma kwa walimu zitaimarika na changamoto zilizopo zitatatuliwa ili walimu waweze kufundisha wanafunzi katika mazingira ya utulivu.

KATUNI

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu


Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Pongezi



Menejimenti na Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)
Tunakupongeza **Prof. Masoud Hadi Muruke** kwa kuaminiwa na
kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt.
Samia Suluhu Hassan kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Tunaahidi kukupatia ushirikiano wa kutosha ili kutimiza
malengo ya kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu.



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

KATIBU WA TSC AFANYA MKUTANO NA WATUMISHI NCHI NZIMA KWA NJIA YA MTANDAO

Na Mwandishi Wetu-Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama ameendesha mkutano na watumishi wa Tume nchini kote kwa njia ya mtandao.

Mkutano huo ulifanyika tarehe 23 Mei 2024 ambapo Katibu wa Tume aliuendesha kutokea jijini Dodoma na Watumishi wa TSC kutoka wilaya zote nchini wakishiriki kwa njia ya wakiwa katika Vituo vyao vya kazi.

Mwl. Paulina akifungua mkutano huo alisema kuwa lengo la kukutana ni kutoa taarifa ya masuala ya Kiutumishi, kuelimishana kuhusu kujiunga na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) katika Tawi la TSC, kupokea changamoto za watumishi na kujadiliana masuala mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji kazi.

Baadhi ya Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu walioko katika Wilaya mbalimbali waliupongeza uongozi wa TSC kwa maandalizi ya mkutano huo ambao umewasaidia kuwasilisha changamoto ambazo zilikuwa zinawakabili.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la TSC, Bw. Francis Gwankisa alimpongeza Katibu wa Tume, Menejimenti na Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa maandalizi mazuri yaliyofanikisha mkutano huo kufanyika kwa watumishi wote wa TSC.

"Kwa niaba ya Watumishi na wanachama wa TUGHE Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu tunawapongeza kwa kuwajali watumishi na kuona umuhimu wa kufanyika kwa mkutano huu.....ni matumaini yetu kuwa mikutano hii itaendelea, hivyo tunatarajia mambo mazuri zaidi," alisema.

Katika hatua nyingine, akifunga

mkutano huo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwalimu Paulina Nkwama aliwataka Watumishi wa TSC kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma wakati wote ili kujiepusha na vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya utumishi huo.

Mwl. Nkwama alisema kuwa Watumishi wanapofanya mawasiliano ni lazima wazingatie taratibu zinazotakiwa kwani kuzipuuza taratibu hizo kunazorotesha utoaji wa huduma jambo ambalo haliwezi kuvumika.

"Kuna lugha ambazo sio za kiutumishi ambazo baadhi yenu mnazitumia..." Mnapofanya mawasiliano zingatieni utaratibu wa mawasiliano katika utumishi wa umma, pia kuna watumishi wanapowasilisha barua wanaanza kuifuatilia kwa kuuliza iko wapi

hadi wakati mwingine wanafuatilia hadi kwa Katibu bila kuzingatia utaratibu bora wa mawasiliano... Masjala pokeeni barua pekeni kwa Katibu na Katibu atapeleka barua inapotakiwa kufanyiwa kazi," alisema

Aliwataka viongozi wanaowasilishiwa barua kuhakikisha wanazifanyia kazi kwa haraka ili wahusika wapate majibu mapema badala ya kusubiri majibu kwa muda mrefu.

Vilevile, Mwl. Nkwama aliwataka watumishi hao kuvaa mavazi yanayoendana na utumishi wa umma kama inavyoelekezwa katika Mwongozo wa Mavazi kwa Watumishi wa Umma kwa mujibu wa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 6 wa mwaka 2020.

"Tunapaswa kuhakikisha tunavaa nguzo kwa mujibu wa mwongozo wa utumishi wa umma...wakati ninapita katika baadhi ya Ofisi nimeona baadhi ya watumishi wanavaa mavazi yasiyoridhisha, unakuta mtu kavaa T-shirts na T-shirts aliyovaa haina hadhi na tena sio ya Tume ...huo sio utaratibu," alisisitiza.

Aidha Mwl. Nkwama aliwataka Watumishi hao kuwa na uhusiano



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiongoza Mkutano uliohusisha watumishi wote wa TSC nchi nzima kwa njia ya mtandao kilichofanyika tarehe 23 Mei, 2024.

KATIBU WA TSC AFANYA MKUTANO NA WATUMISHI NCHI NZIMA KWA NJIA YA MTANDAO

mzuri na umoja katika kutekeleza majukumu ya ofisi huku akionya watumishi ambao wanaendekeza migogoro kazini.

Katibu huyo aliwakumbusha wafanyakazi wa TSC kuwa wako katika Ofisi hizo kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kutoa huduma bora na zinazostahili na sio kuleta ubinafsi katika Ofisi.

"Kuanzia sasa sitasita kuchukua

hatua kwa mtumishi yeyote ambaye hataki kuelewana na wenzake. Sitaki kusikia ofisi fulani kuna watu hawaelewani, kila mmoja ajitahidi kuhakikisha ofisi zetu zinakuwa mfano bora kwa kuwa na umoja, ushirikiano na utendaji kazi mzuri," alisema.

Mwl. Nkwama pia aliwataka watumishi hao kujenga utamaduni wa kuheshimiana kwa viongozi kuwaheshimu wanaowasimamia na vile vile

watumishi kuwaheshimu viongozi wao ili kusaidia utendaji wa kazi kuwa mzuri na kufanya Walimu kupata huduma bora.

Katibu huyo alihitimisha mkutano huo kwa kuwakumbusha Watumishi wa Tume kuwa shughuli zote za utumishi ikiwemo fomu za ruhusa, likizo, mikopo na kufuatilia mafao zitafanyika kwa njia ya mtandao na hivyo hakuna nakala ngumu (hard copy) ambayo itafanyiwa kazi.

Amewataka watumishi kuongeza bidii katika kujifunza matumizi ya huduma mbalimbali zinazotolewa kwa njia ya mtandao ili kuepuka usumbufu usio wa lazima.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Kikao cha Katibu wa Tume na Watumishi wote wa TSC kwa njia ya MTANDAO

"Ninawashukuru watumishi wote wa Tume kwa ushiriki na kufanikisha kikao cha watumishi wote nchi nzima, hakika kikao chetu kimekwenda vizuri. Hoja mlizotoa tutazifanyia kazi ili tuendelee kuboresha mazingira yetu ya kazi kwa lengo la kutoa huduma bora zaidi kwa Walimu. Ninawakumbusha tena tuzingatie Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yetu."

**Mwl. Paulina Nkwama, _ndc_
Katibu, Tume ya Utumishi wa Walimu**



KATIBU WA TSC AFANYA MKUTANO NA WATUMISHI NCHI NZIMA KWA NJIA YA MTANDAO



Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimalizwatu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Zachary Dida akiwasilisha mada wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na watumishi kutoka ofisi zote za Tume hiyo kilichofanyika kwa njia ya mtandao, tarehe 23 Mei, 2024.



Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akiwa katika Mkutano wa Katibu wa TSC na watumishi wa Tume kutoka Ofisi zote (140) za Tume hiyo kilichofanyika kwa njia ya mtandao, tarehe 23 Mei, 2024.



Afisa Utumishi Mwandamizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ambaye pia ni Mwenyekiti wa TUGHE Tarwi la TSC akiwasilisha mada wakati wa Mkutano wa Katibu wa TSC na watumishi kutoka ofisi zote za Tume hiyo kilichofanyika kwa njia ya mtandao, tarehe 23 Mei, 2024.



Mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Watumishi wa TSC kutoka ofisi zote za Tume hiyo kilichofanyika kwa njia ya mtandao, tarehe 23 Mei, 2024 kikiwa kinaendelea.

KATIBU WA TSC AFANYA MKUTANO NA WATUMISHI NCHI NZIMA KWA NJIA YA MTANDAO



Mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Watumishi wa TSC kutoka ofisi zote za Tume hiyo kilichofanyika kwa njia ya mtandao, tarehe 23 Mei, 2024 kikiwa kinaendelea.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AMTEUA PROF. MURUKE KUWA MWENYEKITI WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU

Na mwandishi Wetu - TSC, Dodoma

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan amemteua Prof. Masoud Hadi Muruke kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Prof. Muruke anachukua nafasi ya Prof. Willy Lazaro Komba ambaye muda wake umemalizika.

Taarifa ya uteuzi huo ilitolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus tarehe 15 Mei, 2024.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke.



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

“Asanteni sana kwa salaam za pongezi. Nami naahidi
kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu na kwa msaada wenu
tutafanikisha malengo yetu ya kuwatumikia Walimu
na kukidhi matarajio yao”



Prof. Masoud Hadi Muruke

Baada ya kupokea salam za Pongezi kwa kuteuliwa
kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC)



OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

Pongezi —

" Kwa niaba ya Menejimenti na Watumishi wote wa Tume ya Utumishi wa Walimu ninawapongeza kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, **Mhe. Mohamed O. Mchengerwa** (Mb) kuwa Wajumbe wa Tume. Tunaahidi kuwapa ushirikiano mkubwa ili mtekeleze majukumu yenu ipasavyo kwa ajili ya maendeleo ya Walimu hapa nchini."

Waloteuliwa

Bi. Mariam Gerald Mwanilwa
Bw. Huruma Elias Mageni
Bi. Hadija Mcheka
Bi. Mariam Rashid Haji
Bi. Bahati Shabani Mgongolwa
Bw. Agrey Adelbert Mleli
Bi. Jane Nikusomoka Mtindya
Bw. Lameck Philipo Mahewa



Mwl. Paulina Nkwama ndc

Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

WAZIRI MKENDA AFUNGUA MAONEOSHO YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU JIJINI TANGA

Na Mwandishi wetu – Tanga.

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda tarehe 27 Mei 2024 alifungua Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyoanza tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 jijini Tanga.

Akifungua maonesho hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Waziri Mkenda alisema Wizara hiyo na Taasisi za chini yake imekuwa ikiendesha maadhimisho mbalimbali ikiwemo Maadhimisho ya Kitaifa ya Ubunifu na Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu maarufu kama MAKISATU, Maonesho ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi yaliyokuwa yanaratibiwa kupitia NACTVET na Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyokuwa yanaratibiwa kupitia



Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda akitoa hotuba ya ufunguzi wa Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu tarehe 27 Mei, 2024 jijini Tanga.

TCU.

“Ili kuimarisha ushiriki wa wadau katika ngazi zote ikiwemo mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuongeza hadhi na ufanisi katika matumizi ya rasilimali na uendeshaji kwa

ujumla, maadhimisho yote matatu yameunganishwa na sasa yatajulikana kama Maadhimisho ya Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu,” alisema Waziri Mkenda.

Aliongeza kuwa, maadhimisho hayo yatafanyika kila mwaka na kwa Mkoa utakaopendekezwa, huku akiweka wazi kuwa kwa miaka mitatu mfululizo yatafanyika Mkoani Tanga.

Kwa mujibu wa Mhe. Prof. Mkenda, lengo la Wiki ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu ni kutoa fursa kwa wabunifu, wagunduzi, watafiti, watunga sera, wadau wa maendeleo kushuhudia na Kujivunia (kujifunza au Kujivunia) ujuzi, uzalishaji na matumizi ya teknolojia zinazozalishwa nchini.

“Vile vile, maonesho haya yanatoa fursa kwa wabunifu nchini kuuza bidhaa au huduma zao pamoja na kuonana na wafadhili na wadau watakaoweza kuendeleza na kubiasharisha bunifu zao zaidi,” alisema Waziri Mkenda.

Tume ya Utumishi wa Walimu nayo ni miongoni mwa Taasisi 140 zilizoshiriki maonesho hayo ambayo kwa mwaka 2024 kauli mbiu ni, “Elimu, Ujuzi na Ubunifu kwa uchumi shindani”.



Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda akipata maelezo kutoka kwa mmoja wa washiriki wa Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu tarehe 27 Mei, 2024 jijini Tanga wakati Waziri huyo alipotembelea mabanda kujionea bunifu mbalimbali zilizowasilishwa kwenye maonesho hayo.

WAZIRI MKENDA AFUNGUA MAONEOSHO YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU JIJINI TANGA



Washiriki mbalimbali waliohudhuria ufunguzi wa Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 jijini Tanga.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya akitoa ufafanuzi kwa wateja waliotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu 27 Mei, 2024 jijini Tanga.

WAZIRI MKENDA AFUNGUA MAONEOSHO YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU JIJINI TANGA



Wateja mbalimbali waliotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu tarehe 27 Mei, 2024 jijini Tanga wakipatiwa huduma wakiendelea kupata maelezo. Picha na TSC Tanga

DKT. MSONDE AKUTANA NA KUWAFUNDA WALIMU WA JIJI LA DODOMA JUU YA UMUHIMU WAO KWA NCHI

Na Mwandishi Wetu-TSC - Dodoma

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu) Dkt. Charles Msonde tarehe 27 Mei 2024 amekutana na walimu wa shule za Msingi na Sekondari kutoka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kuwapa mbinu za kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wao.

Akizungumza na Walimu hao, Naibu Katibu Mkuu huyo alisema Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inawathamini sana walimu nchini kwa kuwa wanafanyakazi nzuri.

Alisema kuwa Serikali kwa kutambua na kuthamini mchango wa Walimu katika kuleta maendeleo nchini ndio maana imeamua kushughulikia changamoto ambazo zilikuwa zikiwakabili ikiwemo za kuchewa kupandishwa madaraja na kutolipwa mapunjo ya mishahara na stahili za fedha za likizo.

"Rais anawapenda sana walimu...Serikali ya Awamu ya Sita inawapenda sana walimu na inawathamini na ndio maana inajitahidi kushughulikia changamoto zinazowakabili," alisema Naibu Katibu Mkuu huyo.

Dkt. Msonde alisisitiza kutokana na dhamira ya dhiti ya Serikali katika kujali maslahi ya walimu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Tawala Mhe. Mohamed Mchengerwa ameagiza kuwa ikifika mwezi Julai hataki kusikia tena changamoto zinazohusu kuchelewa kupandishwa madaraja kwa walimu.

Aliongeza kuwa Walimu wanafanya kazi kubwa nchini ya kulea na kuwapa ujuzi watu mbalimbali ambao hatimaye unawasaidia wao binafsi kupata maendeleo na Taifa kwa ujumla.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Dkt. Charles Msonde akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Jiji la Dodoma tarehe 27 Mei 2024 katika ukumbi wa Shule ya Msingi ya Mtakatifu Gaspar jijiji Dodoma wakati akiwapa mikakati mabadiliko ya maboresho katika utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa Sekondari na Shule za Msingi.

"Tunapooona Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi, Wanasheria, Wahandisi, Wafanyabiashara hawajawa hivyo walivyo bila kupitia katika mikono ya Walimu...Walimu ni watu muhimu katika malezi na kuwaumba watumishi," alisema Dkt. Msonde.

Katika hatua nyingine Naibu Katibu Mkuu nabaadhiya viongozi walioongozana naye akiwemo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu waliweza kutoa namba zao za simu za mikononi ili ziwawezesha walimu kuwasilisha changamoto zinazowakabili kwa ajili ya kuzitafutia ufumbuzi.

Akizungumzia masuala ya mawasiliano, Naibu Katibu Mkuu aliwaasa viongozi mbalimbali kuhakikisha wanapopokea barua, ujumbe na simu kutoka kwa wanaowatumikia kuhakikisha wanawajibu kwa kwa haraka na kupokea ushauri unaolenga kuboresha utoaji huduma kwa walimu.

Aidha, Dkt. Msonde aliwataka walimu wenye changamoto kupitishia kwa Maafisa Elimu wa Shule za Msingi na Sekondari na wao ndio wanapaswa kupeleka

barua na vielelezo vya Walimu kwa Maafisa Utumishi ili kuepuka kupata majibu yanayowakatisha tamaa.

Wakati huo huo Dkt. Msonde aliwataka walimu hao kuancha tabia ya kufanya kazi kwa mazoea badala yake wanatakiwa kutoa elimu kwa ubunifu na kuwaacha kuwakatisha tamaa wanafunzi hata katika masomo ambayo wanadhani kuwa ni magumu ili kuwawezesha kufanya vizuri.

Katika ziara hiyo Naibu Katibu Mkuu aliongoza na Viongozi wengine akiwemo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais TAMISEMI Dkt. Emmanuel S. Shindika, Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, anayesimamia Elimu ya Awali na Msingi, Mwl. Susan Nussu, Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Masuala Maalum Tamisemi, Mwl. Ernest Hinju, Mkurugenzi Msaidizi Sekondari, kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bi Khadija Mcheka na Afisa Elimu Mkoa wa Dodoma Bw. Vicent Kayombo.

**DKT. MSONDE AKUTANA NA KUWAFUNDA WALIMU WA
JIJI LA DODOMA JUU YA UMUHIMU WAO KWA NCHI**

Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Emmanuel S. Shindika akitoa maelezo ya awali kabla ya kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Dkt. Charles Msonde kuzungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Jiji la Dodoma tarehe 27 Mei 2024 katika ukumbi wa Shule ya Msingi ya Mtakatifu Gaspar jijiji Dodoma.



Baadhi ya Walimu kutoka Tarafa za Jiji la Dodoma wakisikiliza maelekezo ya Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Elimu), Dkt. Charles Msonde tarehe 27 Mei 2024 katika ukumbi wa Shule ya Msingi ya Mtakatifu Gaspar jijiji Dodoma alipokuwa akiwapa mbinu za kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa Sekondari na Shule za Msingi.



MKUU WA MKOA WA TANGA AIPONGEZA TSC KWA KUPANDISHA VYEO WALIMU NA KUJENGA MFUMO WA TSCMIS

Na Mwandishi wetu – Tanga.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Batilda Burian ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kusimamia vyema walimu hususan katika eneo la kupandisha vyeo pamoja kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa kusimamia masuala ya utumishi wa walimu ujulikanao kama Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS).

Pongezi hizo amezitoa tarehe 30 Mei, 2024 wakati alipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yanayofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga.

Kiongozi huyo alisema kuwa kwa sasa walimu wamekuwa na utulivu mkubwa baada ya kuona changamoto zao hususan za upandishwaji wa vyeo zimefanyiwa kazi na wanaendelea kupata haki zao.

"Tunawapongeza Tume kwa kazi nzuri mnayoifanya, siku za nyuma kilio kikubwa cha walimu kilikuwa ni kucheleweshwa kupandishwa vyeo. Lakini kwa sasa tunaona mmejithahidi kuwapandisha walimu wengi, jambo ambalo limesaidia kuongeza morali ya walimu katika kufundisha wanafunzi. Na hii ndiyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha kila mwalimu anapata haki yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu," alisema Kiongozi huyo.

Mhe. Burian aliongeza kuwa Mfumo wa TSCMIS utasaidia sana walimu kuondoa usumbufu wa kuondoka kwenye vituo vya

kazi kwa ajili ya kwenda kutafuta huduma katika ofisi mbalimbali, hivyo aliahidi kuwa katika Mkoa wa Tanga atafanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha walimu wote wanajisajili kwenye mfumo huo.

Pamoja na hayo, Mkuu huyo wa Mkoa aliishauri TSC kuendelea kusimamia kwa karibu masuala ya maadili ya walimu ikiwa ni pamoja na walimu kutoadhibu wanafunzi kinyume na utaratibu, jambo linalofanya wanafunzi kuchukia shule.

Alisema katika kutekeleza hilo, TSC inapaswa kuendelea kutoa elimu kwa walimu mara kwa mara ili watekeleze wajibu wao kwa kuzingatia Miiko na Maadili ya kazi ya ualimu.

"Tunatamani wanafunzi waone shuleni ni sehemu salama ya kukimbilia, tunataka wapende shule. Sasa kama kuna mwalimu anawachapa wanafunzi kupita kiasi ni wazi kwamba mwanafunzi atachukia shule. Kuna adhabu

nyingi tu za kumpa mwanafunzi pale inapohitajika ambazo zinamfundisha na hazimfanyi achukie shule. Tunaomba muendeleo kuwaelimisha walimu wetu kuzingatia taratibu hizo," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu (TSC), Mwl. Fatuma Muya alimshukuru Mkuu huyo wa Mkoa kwa kutembelea banda la TSC na kuahidi kuwa Tume hiyo itaendelea kuhudumia walimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu ili waendeleo kufundisha wanafunzi katika mazingira ya utulivu.

Mwl. Muya alimpatia kiongozi huyo nyaraka kadhaa ikiwemo Kitabu cha Ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu na Kitabu cha Ufafanuzi wa Masuala Muhimu yaliyomo katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 na Kanuni zake za mwaka 2016.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Batilda Burian akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 30 Mei, 2024 alipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga.

MKUU WA MKOA WA TANGA AIPONGEZA TSC KWA KUPANDISHA VYEO WALIMU NA KUJENGA MFUMO WA TSCMIS

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Batilda Burian akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) tarehe 30 Mei, 2024 alipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Batilda Burian (kustoto) akipokea maelezo kuhusu Mfumo wa Kielektroniki wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) kutoka kwa Afisa TEHAMA wa TSC, Bw. Pastory Munyaki (kulia) tarehe 30 Mei, 2024 wakati Mkuu huyo wa Mkoa alipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mhe. Balozi Batilda Burian (kulia) akipokea vitabu vya ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya Utumishi wa Walimu kutoka kwa Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa TSC, Mwl. Fatuma Muya tarehe 30 Mei, 2024 katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga.

MWL. NKWAMA AWAFAKUNA WALIMU WA WILAYA YA CHAMWINO

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Chamwino tarehe 28 Mei, 2024.

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama tarehe 28 Mei, 2024 amekutana na walimu wa shule za Msingi na Sekondari kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma kuwapa mbinu za kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi kwa ajili ya kuleta mabadiliko katika sekta ya elimu.

Akizungumza na Walimu hao, Mwl. Nkwama alisema Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inawapenda sana walimu na ndio maana inaendelea kushughulikia changamoto zinazowakabili.

Alisema kuwa Serikali kwa kutambua na kuthamini mchango wa Walimu katika kuleta maendeleo nchini, imeamua kushughulikia changamoto ambazo waliziwasilisha ikiwemo za kuchelewa kupandishwa madaraja na kutolipwa mapunjo ya mishahara na stahili za fedha za likizo.

Mwl. Nkwama alisisitiza kuwa hata Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Tawala Mhe. Mohamed Mchengerwa yuko karibu na

walimu na hataki kusikia kuwa changamoto zao hazitafutiwi ufumbuzi.

Alisemakuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeamua kuhakikisha kuwa Walimu wanafanya kazi ya kulea na kuwapa ujuzi Watoto wakiwa hawana changamoto zinazowakabili na ndio maana imekusudia kupandisha madaraja ya walimu takriban 54,000 kwa njia ya mserekeru na wengine 52,000 kwa njia ya kawaida kwa wale wenye sifa.

Kuhusu madai ya malimbiko za mshahara (arrears) baada ya kupanda madaraja na madai ya fedha za likizo, aliwaelekeza Maafisa Elimu Sekondari na

Msingi kushirikiana na Maafisa Utumishi ili walimu wapate haki yao.

Aidha kwa upande wa likizo na madai ya uhamisho, aliwataka Maafisa Elimu hao kushughulikia kwa weledi, mtumishi anayeanza Kwenda likizo alipwe kabla ya aliyefuata.

Akizungumzia uwajibikaji kwa walimu, Mwl. Nkwama aliwataka kuhakikisha wanaleta mabadiliko makubwa katika sekta ya elimu nchini kwa kuwa wabunifu na kuacha kufundisha kwa mazoea.

“Walimu lazimu muwe wabunifu kwa kuwa nyie ndio mmekaa kwenye seat ya kuendesha gari la elimu...tuwalee Watoto na tuwape ujuzi kwa ajili ya maendeleo yao ya baadae na Taifa,” alisema Mwl. Paulina.

Ziara hiyo ya kukutana na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari inaendelea katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati ya elimu nchini na kuwapongeza walimu kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya ya kuleta mageuzi makubwa wanayoendelea nayo, na kwamba Serikali ipo pamoja na walimu katika kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu nchini.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwapungia mkono walimu wakati alipokuwa akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Chamwino tarehe 28 Mei, 2024.

MWL. NKWAMA AWAFUNDA WALIMU WA WILAYA YA CHAMWINO



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Bw. Tito Mganwa akitoa neno la shukurani mara baada ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu kumaliza hotuba yake kwa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya hiyo.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali kuimba wimbo wa walimu wa Mkoa wa Dodoma tarehe 28 Mei, 2024 katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Chamwino kabla ya kuanza mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari.



Baadhi ya Walimu wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) wakati akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Chamwino leo tarehe Mei, 2024.



Baadhi ya Walimu kutoka Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya ya Chamwino wakiwa katika picha ya pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) tarehe 28 Mei 2024 baada ya mkutano.



Baadhi ya Walimu kutoka Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya ya Chamwino wakiimba wimbo wa Mkoa wa Dodoma kabla ya kuanza kwa mkutano kati yao na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) tarehe 28 Mei 2024.

WAZIRI MCHENGERWA AITAKA TSC KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI ZOTE KUHAKIKISHA MICHANGO YA WALIMU INAWASILISHWA KWENYE MFUKO YA HIFADHI YA JAMII KWA WAKATI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa akiwa katika kikao chake na baadhi Viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), tarehe 15 Mei, 2024.

Na Mwandishi Wetu - TSC, Dodoma

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa ameitaka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kushirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini ili kutatua changamoto zinazowakabili walimu ikiwemo ucheleweshaji wa kuwasilisha michango ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Waziri Mchengerwa ametoa agizo hilo tarehe 15 Mei, 2024 jijini Dodoma wakati wa kikao chake na baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) baada ya viongozi wa TSC kuwasilisha taarifa ya zoezi maalum la

uchambuzi wa changamoto za upandishaji wa madaraja vyeo kwa walimu.

Mhe. Mchengerwa alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kuondoa changamoto wanazokabiliana nazo walimu



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (kulia) akiwa katika kikao chake na baadhi Viongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), tarehe 15 Mei, 2024.

wakati wanapofuatilia mafao yao kwenye mifuko na kukuta kuwa baadhi ya Waajiri wameshindwa kuwasilisha michango ya watumishi katika Mfuko wa PSSSF.

Aidha, Waziri huyo aliongeza kuwa ni vema TSC ione uwezekano wa kukutana na Walimu mara kwa mara na kutatua changamoto zinazowakabili ikiwemo kujenga uelewa kuhusiana na magonjwa ya afya ya akili.

Mhe. Mchengerwa aliagiza TSC kwa kushirikiana na Wakurugenzi Watendaji kuandaa orodha ya walimu waliopo karibu kustaafu na kuwapa elimu ya maandalizi ya kustaafu ili kuwawezesha kuendelea kuwa na Maisha bora hata maada ya kuhitimisha utumishi wao.

Katika hatua nyingine Waziri Mchengerwa alitaka kiandaliwe kikao cha pamoja kati ya Ofisi yake, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kwa ajili ya majadiliano kuhusu uboreshaji maslahi na utatuzi wa changamoto za walimu.

Aidha, Mhe. Mchengerwa aliitaka TSC kuweka mipango Madhubuti ya kujenga Ofisi za Wilaya ili kukabiliana na ukosefu wa Ofisi kwa Watumishi wa TSC katika ngazi ya wilaya.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWAPA TABASAM WALIMU 578 WILAYA YA MKALAMA KWA KUWAPANDISHA VYEO

Na Mwandishi wetu – Mkalama.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan walimu 578 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Mkalama wamepandishwa vyeo ikiwa ni moja ya jitihada za Serikali za kushughulikia maslahi ya walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkalama, Bw. John Kingu alipotembelewa na maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Bw. Kingu alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Mkalama zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

"Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2021/2022 tulipandisha vyeo walimu 240, mwaka 2022/2023 tulipandisha walimu 108 na mwaka 2023/2024 tumepandisha vyeo walimu 230, hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu," alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Mkalama, Kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu

wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Aidha Kingu aliliendelea kueleza kuwa, katika miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia, jumla ya walimu 258 wameajiriwa na hivyo TSC Wilaya ya Mkalama kufikisha idadi ya walimu 1,047 ambao inawasimamia ambao wanafundisha katika shule za msingi na sekondari 119.

Alisema jambo jingine ambalo Serikali ya Awamu ya Sita imewasaidia TSC Wilaya ya Mkalama ni pamoja na kuwapatia vifaa vya ofisi (vitajwe japo kwa uchache kama mfano) na usafiri wa pikipiki ambao umewawekea mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Kingu alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Mkalama imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu

wa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

"Tumefanikiwa kutembelea shule 119 ambapo 98 ni za msingi na 21 ni za sekondari. Katika ziara hizo tumefanikiwa kutoa ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji kazi katika Utumishi wa Walimu katika shule zote. Jitihada zote hizi ni kusaidia walimu kutekeleza majukumu yao bila kukiuka miiko ya kazi yao," alisema.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

"Katika kipindi cha miaka mitatu, mashauri ya nidhamu 5 yalifunguliwa ambapo walimu 3 waliopatikana na hatia na kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi. Walimu 2 hawakupatikana na hatia na hivyo waliachiwa huru," alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkalama, Bw. John Kingu akielezea mafanikio na hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo akiwa ofisini kwake hivi karibuni.

**RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWAPA TABASAM WALIMU
578 WILAYA YA MKALAMA KWA KUWAPANDISHA VYEO**

Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkalama , Bw. John Kingu akielezea mafanikio na hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo akiwa ofisini kwake hivi karibuni.



Afisa Ajira wa TSC Wilaya ya Mkalama Bw. Venance Lutengano, akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya ajira za Walimu katika Wilaya hiyo ofisi kwake.



Watumishi wa TSC Wilaya ya Mkalama, Bw. John Kingu (kushoto) na Bw. Venance Lutengano wakiwa katika picha ya pamoja katika ofisi za TSC Wilaya ya Mkalama hivi karibuni.

TSC WAJADILIANA NA EDUCATE FURSA ZA KUSHIRIKIANA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakiongozwa na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama wamekutana na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Educate, Bw. Kamari alisema lengo la kuangalia maeneo ya kushirikiana kwenye kuwajengea uwezo walimu.

Kikao hicho kimefanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu na kuhudhuria na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya na Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, Bi. Evodia Pangani.

Akizungumza katika kikao hicho, Katibu wa Tume ya Utumishi

wa Walimu (TSC) Mwl. Nkwama alisema ipo haja ya kuangalia uwezekano wa kushirikiana katika maeneo ya kuwajengea uwezo walimu wakuu katika masuala ya Uongozi ili waweze kuwasimamia Walimu wenzao ipasavyo.

Mwl. Nkwama aliongeza kuwa TSC ina jukumu la kukusanya takwimu za walimu na kuishauri Serikali juu ya maslahi ya walimu, pengo la upungufu wa walimu ambao wanapaswa kuajiriwa kwa kuzingatia aina ya masomo na shule ambazo zinakabiliwa na upungufu.

Aidha, Katibu huyo alisema katika kusimamia masuala ya walimu wamekuwa wakishirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wadhibiti Ubora, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) na Kamshna wa Elimu.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Educate, Bw. Kamari alisema lengo la ziara yake katika Ofisi za TSC ni kuangalia fursa zilizopo na vipaumbele ambavyo Shirika hilo linaweza kuunga mkono katika utoaji wa huduma kwa walimu kwenye masuala ya kuwajengea uwezo walimu.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini Bi. Evodia Pangani alisema ni vema kuangalia uwezekano kujumuisha katika Mitaala ya Ufundishaji wa Walimu kwa ngazi ya Vyuo Vikuu nchini mafunzo ya maadili kwa walimu kwa ajili ya kuwasaidia wahitimu wanapokuwa wameajiriwa kuepuka vitendo vinavyoweza kuwasababisha kuingia katika matatizo.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akiongoza kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya TSC na Shirika lisilo la Kiserikali la Educate kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.



TSC WAJADILIANA NA EDUCATE FURSA ZA KUSHIRIKIANA



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu TSC, Mwl. Fatuma Muya akizungumza wakati wa kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Shirika lisilo la Kiserikali la Educate kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Educate, Bw. Kamanda Kamiri akizungumza wakati wa kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Shirika lisilo la Kiserikali la Educate kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akiagana na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Educate, Bw. Kamanda Kamiri mara baada ya kuhitimisha kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya TSC na Shirika lisilo la Kiserikali la Educate kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.

Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini TSC, Bi. Evodia Pangani akizungumza wakati wa kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na Shirika lisilo la Kiserikali la Educate kilichofanyika tarehe 22 Mei, 2024 katika Ofisi za Katibu wa TSC jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la Educate, Bw. Kamanda Kamiri (wa pili kutoka kulia). Pichani, wengine ni Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya TSC (wa kwanza kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini TSC, Bi. Evodia Pangani (wa kwanza kulia).

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ASHUSHA NEEMA WALIMU WAPATAO 2,180 WILAYA YA SINGIDA KWA KUWAPANDISHA VYEO

Na Mwandishi wetu – Singida

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan walimu 2,180 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Singida wamepandishwa vyeo ikiwa ni moja ya jitihada za Serikali za kushughulikia maslahi ya walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Singida, Bw. Amos Daniel Kimu alipotembelewa na maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Bw. Kimu alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Wilaya ya Singida zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2020/2021 walipandisha vyeo walimu 75, mwaka 2021/2022 walipandisha walimu 1,332 na mwaka 2022/2023 tumepandisha vyeo walimu 773, na walimu 52 walibadilishwa kazi,” hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu nchini alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu

Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Singida Manispaa na Wilaya kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Aidha Kimu aliendelea kueleza kuwa, katika miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia, jumla ya walimu 272 wameajiriwa katika Halmashauri mbili. Manispaa ya Singida waliajiriwa 38 na Halmashauri ya Wilaya ya Singida waliajiriwa walimu 234 katika kipindi cha miaka mitatu.

Alisema jambo hilo limesaidia kuongeza nguvu kwa walimu waliokuwepo ambao wanahudumia shule za Msingi 1,632 na Sekondari 861 kwa Halmashauri zote mbili za Wilaya ya Singida.

Bw. Kimu aliongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita kupitia jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa TSC Wilaya ya Singida tumefaidika na mambo makubwa yafuatayo:- kulipwa madeni (yapi hayo eleza kwa uchache), kulipwa stahiki (zipi?) na kupatiwa vifaa vya ofisi (kama vile ...) na usafiri wa pikipiki ambao umewawekea mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa ari na moyo.

“Tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kuipa sekta ya elimu kipaumbele na hasa walimu ili lengo la kuwa na jamii iliyoelimika na kufikia maendeleo ya kweli katika Nchi yetu litimie,” alisema.

Akizungumzia suala la maadili

na nidhamu kwa walimu, Bw. Kimu alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Singida imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

“Tumefanikiwa kuwa na vikao 10 kwa kushirikiana na Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri zote mbili lengo ikiwa ni kutoa elimu na ufafanuzi juu ya Sheria, Kanuni na Maadili ya walimu ili kuwakinga wasijiingize katika makosa ambayo yanaweza kuathiri utumishi wao. Tumefanya ziara katika shule zipatazo 113 na kugawa vitabu kwa wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya ya Singida. Jitihada zote hizi ni kusaidia walimu kutekeleza majukumu yao bila kukiuka miiko ya kazi yao,” alisema.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

“Katika kipindi cha miaka mitatu, mashauri ya nidhamu 55 yalifunguliwa na kuamuliwa ambapo walimu 30 waliopatikana na hatia na kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi. Walimu 25 hawakupatikana na hatia na hivyo waliachiwa huru,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Singida inahudumia Halmashauri mbili ambazo ni Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ASHUSHA NEEMA WALIMU WAPATAO 2,180 WILAYA YA SINGIDA KWA KUWAPANDISHA VYEO



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Singida, Bw. Amos Kimu akielezea mafanikio na hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo akiwa ofisini kwake hivi karibuni.

Afisa wa Nidamu wa TSC Wilaya ya Singida Mwalimu. Flora Mushi, akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya ajira za Walimu katika Wilaya hiyo ofisi kwake.



Watumishi wa TSC Wilaya ya Singida, Amos Kimu (kulia) na Mwalimu Flora Mushi (kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja katika ofisi za TSC Wilaya ya Singida hivi karibuni.

MENEJIMENTI ZA TAASISI ZA OR TAMIMSEMI ZATAKIWA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA PEPMIS KWA WATUMISHI WA CHINI

**Na Mwandishi Wetu -TSC,
Dodoma**

Menejimenti za Taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) zimetakiwa kuwawasaidia na kuwasimamia watumishi walio chini yao katika kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma -PEPMIS/PIPMIS kwa kuzingatia maelekezo ili kuleta ufanisi.

Agizo hilo limetolewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI anayeshughulikia Afya, Dkt. Wilson M. Charles tarehe 15 Mei, 2024 wakati akifungua mafunzo ya siku tatu yanayohusu ufuatiliaji wa Matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS/PIPMIS) kwa Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakurugenzi Wasaidizi walioko katika Taasisi zilizoko chini ya OR – TAMISEMI.

Alisema kuwa mfumo huo umejengwa katika misingi wa kuwasaidia watumishi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika shughuli za umma na vilevile kupata huduma mbalimbali ikiwemo kupata mikopo katika Taasisi za Fedha na kufuatilia uhamisho kwa urahisi bila urasimu.

Dkt. Charles aliongeza kuwa matumizi ya Mfumohuoyamesaidia kudhibiti na kuondoa watu ambao waliokuwa wakiwatapeli baadhi ya watumishi kwa kuwaomba fedha kwa kiwango cha kuanzia shilingi milioni moja na kuendelea kwa madai ya kuwa watawatafutia uhamisho huku wakighushi saina za Viongozi ikiwemo Katibu Mkuu ofisi ya Rais TAMISEMI na Katibu Mkuu (UTUMISHI).



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya Dkt. Wilson M. Charles (katikati) akiwaongoza Wajumbe wa Menejimenti kutoka Taasisi zilizoko chini ya TAMISEMI kumkumbuka mmoja wa Machampioni wa kutoa mafunzo ya Mfumo upimaji wa Watumishi aliyefariki dunia hivi karibuni kabla ya kufungua mafunzo ya zoezi la ufuatiliaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS/PIPMIS) tarehe 15 Mei, 2024 jijini Dodoma. Wengine katika picha ni Mkurugenzi wa Utawala wa Utumishi wa Umma - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bi. Felister Emmanuel Shuli (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu – Ofisi ya Rais TAMISEMI, Bw. Stanley Ngozi (kulia).

Alisema hali hiyo imesababisha madhara mbalimbali ikiwemo usumbufu kwa watumishi ambao walikuwa wakitapeliwa kwa kuhamia katika Kituo ambacho walikwenda bila utaratibu huku mishahara yao ilibaki katika vituo vyao vya awali.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala wa Utumishi wa Umma - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bi. Felister Emmanuel Shuli aliwataka viongozi wa Menejimenti za Taasisi zote ambazo ziko chini ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa watumishi wote ambao hawajasajiliwa katika Mfumo huo kutekeleza jukumu hilo ili kuepuka

kuondolewa katika utumishi wa umma kwa kudhaniwa kuwa ni watumishi hewa.

Aliongeza kuwa kuanza kwa Mfumo kumesaidia kuwabaini na kuwachukulia hatua baadhi ya Watumishi wasiozingatia maadili waliokuwa wakishirikiana na vishoka kuchukua fedha za watumishi kuanzia kiasi cha shilingi milioni moja hadi shilingi milioni tano kwa madai ya kuwatafutia uhamisho ili waende Taasisi ambazo wanadhani kwa maoni yao zina maslahi mazuri.

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu ni miongoni mwa Taasisi ambazo zimeshiriki mafunzo hayo wakiongozwa na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina Nkwama.

MENEJIMENTI ZA TAASISI ZA OR TAMIMSEMI ZATAKIWA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA PEPMIS KWA WATUMISHI WA CHINI



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa anayeshughulikia Afya Dkt. Wilson M. Charles (katikati) akitoa hotuba ya kufungua mafunzo ya zoezi la ufuatilia wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS/PIPMIS) kwa Wajumbe wa Menejimenti kutoka Taasisi zilizo chini ya TAMISEMI tarehe 15 Mei, 2024 jijini Dodoma. Wengine katika picha ni Mkurugenzi wa Utawala wa Utumishi wa Umma - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bi. Felister Emmanuel Shuli (kushoto) na Kaimu Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu - OR TAMISEMI, Bw. Stanley Ngozi (kulia).

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiwa katika mafunzo ya zoezi la ufuatilia wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS/PIPMIS) tarehe 15 Mei, 2024 jijini Dodoma.



Wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika mafunzo ya zoezi la ufuatilia wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS/PIPMIS) tarehe 15 Mei, 2024 jijini Dodoma.

MWL. PAULINA: WALIMU TUMPE RAIS SAMIA MAUA YAKE KWA UBORESHAJI WA ELIMU NA MIRADI YA ELIMU

Na Mwandishi Wetu-Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama amewataka Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kutambua mambo mazuri aliyowafanyia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na kumpongeza kwa juhudi zake za kuboresha elimu na mafunzo wa walimu nchini kupitia miradi mbalimbali.

Ametoa kauli leo tarehe 29 Mei, 2024 wakati mkutano na Walimu kutoka Halmashauri za Wilaya ya Kongwa na Mpwapwa alipokuwa akielezea jinsi Serikali anayoiongoza ilivyojitahidi kuondoa kero na changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu na sekta ya elimu kwa ujumla nchini.

Mwl. Paulina alisema kuwa Serikali katika mwaka ujao wa fedha mara baada ya taratibu za kiutumishi itawapandisha madaraja walimu 54,000 kwa njia ya mserereko waliocheleweshwa na wengine 52,000 kwa njia ya kawaida kwa wale wenye sifa.

Alisema kuwa sanjari na hilo Serikali inayoongozwa na Rais Mhe. Dkt. Samia imeamua kushughulia changamoto ya walimu ambao wanadai mapunjo ya mishahara(Arrears) baada ya kupandishwa madaraja kwa



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Mwl. Paulina Nkwama(katikati) akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Mpwapwa leo tarehe 29 Mei, 2024.

kuhakikisha wanalipwa na stahili za fedha zao ikiwemo wale wanadai fedha za likizo.

Mwl. Paulina alisema kuwa Rais Samia amejipambanua kuwa anawapenda walimu kwa jinsi ambavyo ameweka mazingira mazuri ya walimu kutoa elimu kwa kuondoa changamoto zao na ikiwemo kutoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu.

Aliongeza kuwa ushahidi wa juhudi hizo unajionyesha kupitia fedha ambazo amepeleka katika Wilaya mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbinu ziwemo bilioni 5 ambazo alitoa kwa Wilaya

ya Mpwapwa kwa ajili ya Sekondari na Shule za Msingi.

Mwl. Paulina alisema kuwa kutokana na juhudi hizo walimu nao wanapaswa kuongeza juhudi katika kuwafundisha Watoto kwa kuwalea katika maadili, uzalendo, utu mwema ili wapate ujuzi wa kuleta maendeleo yao na taifa kwa ujumla kama zawadi kwake.

Ziara hiyo ya kukutana na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari inaendelea katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutoa mikakati ya kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu nchini.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Mwl. Paulina Nkwama(katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali kuimba wimbo wa walimu wa Mkoa wa Dodoma leo tarehe 29 Mei, 2024 katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Francis ya Wilayani Kongwa kabla ya kuanza mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari.

MWL. PAULINA: WALIMU TUMPE RAIS SAMIA MAUA YAKE KWA UBORESHAJI WA ELIMU NA MIRADI YA ELIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Mwl. Paulina Nkwama(katikati) akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kongwa leo tarehe 98 Mei, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Mwl. Paulina Nkwama(katikati) akisisitiza jambo wakati akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kongwa leo tarehe 98 Mei, 2024.



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kongwa wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu(TSC) Mwl. Paulina Nkwama(hayupo katika picha) leo tarehe 29 Mei, 2024 katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana na Mtakatifu Francis Kongwa wakati wa mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN ASHUSHA NEEMA KWA WILAYA YA IKUNGI



Watumishi wa TSC Wilaya ya Ikungi, Bi. Stella Mollel (kushoto), Mwalimu Johari Kapaya na Bw. Richard John (katikati) wakiwa katika picha ya pamoja katika ofisi za TSC Wilaya ya Ikungi hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu – Ikungi.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan walimu 1,256 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Ikungi wamepandishwa vyeo ikiwa ni moja ya jitihada za Serikali za kushughulikia maslahi ya walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ikungi, Bi. Stella Mollel alipotembelewa na maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Bi. Stella alieleza pia katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia walimu 341 wameajiriwa katika Shule za Msingi na Sekondari

ambapo kati ya hao shule za Msingi ni 258 na Sekondari ni 83.

Alisema kuwa katika kipindi hicho walimu 108 wamebadilishwa vyeo ikiwa walimu 84 ni kutoka shule za msingi na Sekondari 24 na kuongeza kuwa hatua hiyo imesaidia kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

Aidha Bi. Stella aliendelea kueleza kuwa, Wilaya ya Ikungi imeendelea kuutumia mfumo wa TSCMIS tangu ulipoanzishwa mwaka 2023 ambapo walimu 168 wa ajira mpya wamesajiliwa na kuwasaidia walimu 954 sawa na asilimia 53 kujaza na kupakia nyaraka zinazohusu madaraja kwenye mfumo.

“Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia kumekuwepo na ongezeko na uboreshaji wa masuala yanayohusu maendeleo ya walimu husasani

katika ajira, upandishaji vyeo na kubadilishwa vyeo. katika kufanya hivyo, maslahi na stahiki za walimu zimeguswa na kupewa kipaumbele kwa kiasi kikubwa” alisema.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ikungi imeendelea kuwafikia walimu katika ziara shuleni kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

“Tumefanikiwa kuwa na ziara katika shule zilizopo katika Kata 28 za Wilaya ya Ikungi ambapo walimu 1,657 wamefikwa na elimu juu ya mambo yanayohusu maadili na nidhamu na kuweza kugawa jumla ya vitabu 125 vinavyotoa ufafanuzi wa kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu.

Aliendelea kuelezea pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

“Katika kipindi cha miaka mitatu, mashauri ya nidhamu 16 yalifunguliwa ambapo kati ya hayo 11 yalihitimishwa na kutolewa adhabu kulingana na miongozi na kanuni. Mashauri Matano (5) yamepokelewa hivi karibuni bado hayajaanza kusikilizwa kwa sababu ya kusubiri Kamati,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Ikungi ina jumla ya shule za Msingi 134 na Sekondari 34.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Ikungi, Bi. Stella Mollel akielezea mafanikio na hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo akiwa ofisini kwake hivi karibuni.



Afisa wa Nidhamu wa TSC Wilaya ya Ikungi Mwalimu Johari Kapaya, akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya ajira za Walimu katika Wilaya hiyo ofisini kwake.



Afisa Ajira TSC Ikungi Bw. Richard John akitoa ufafanuzi kuhusu hali ya ajira za Walimu katika Wilaya hiyo ofisi kwake.

WALIMU JIJINI TANGA WATUMIA MAONESHU YA KITAIFA YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA TSCMIS

Na Mwandishi wetu – Tanga.

Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliitembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika jijini Tanga na kupatiwa elimu ya namna ya kujisajili kwenye mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS).

Wengi wa walimu waliitembelea banda hilo siku ya Jumanne tarehe 28 Mei, 2024 walieleza kuwa wameshindwa kukamilisha usajili wao kutokana na changamoto mbalimbali na hivyo kuchukua hatua ya kufika katika maonesho hayo ili waweze kukamilisha zoezi hilo.

"Nimejaribu kujisajili kwenye mfumo wa TSCMIS lakini nilifika sehemu nikakwama, nilipoambiwa TSC wapo kwenye maonesho nikasema lazima nifike kwenye banda ili niweze kusaidiwa," alieleza mmoja wa walimu waliitembelea banda la TSC.

Walimu wote waliofika kwenye banda hilo walihudumiwa na kusaidiwa kukamilisha zoezi la kujisajili katika mfumo huo unaolenga kurahisisha upatikanaji wa huduma za kiutumishi kwa walimu.

Kwa upande wa Maafisa wa TSC wanaotoa huduma katika banda hilo walisema walimu wengi wanapata changamoto za kukamilisha usajili kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha wa namna ya kutumia mfumo huo.

Hivyo, pamoja na kusaidiwa kukamilisha kujisajili, walimu hao walipewa elimu ya kutosha



Afisa TEHAMA wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Pastory Munyaki (kushoto) akiwaelekeza walimu namna ya kutumia Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 jijini Tanga.

ya namna ya kuingia na wakawaelimishe walimu wengine kutumia mfumo huo ili nao katika maeneo yao.

**WALIMU JIJINI TANGA WATUMIA MAONESHU YA KITAIFA YA ELIMU,
UJUZI NA UBUNIFU KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA TSCMIS**

Afisa TEHAMA wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Pastory Munyaki (kushoto) akiwaelekeza walimu namna ya kutumia Mfumo wa Teachers' Service Commission Management Information System (TSCMIS) katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 jijini Tanga.



Afisa Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Josephine Chilongozi akiwasikiliza walimu waliotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 jijini Tanga.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AGUSA MASLAHI YA WALIMU WA WILAYA YA MANYONI

**Na Mwandishi wetu –
Manyoni.**

Katikakipindichamiaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan walimu 1,342 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Manyoni wamepandishwa vyeo ikiwa ni moja ya jitihada za Serikali za kushughulikia maslahi ya walimu.

Hayo yameelezwa na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Manyoni, Bi. Hawa Rajab alipotembelewa na maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Bi. Hawa alieleza pia katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Samia walimu 379 wameajiriwa katika Shule za Msingi na Sekondari ambapo kati ya hao shule za Msingi ni 264 na Sekondari ni 115

Alisema kuwa katika kipindi hicho walimu 13 wamebadilishiwa vyeo ikiwa walimu 09 ni kutoka shule za msingi na Sekondari 04 na

kuongeza kuwa hatua hiyo imesaidia kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

Aidha Bi. Hawa aliendelea kueleza kuwa, Wilaya ya Manyoni imeendelea kuutumia mfumo wa TSCMIS tangu ulipoanzishwa mwaka 2023 walimu 183 wa ajira mpya wamesajiliwa na kuwasaidia walimu 505 sawa na asilimia 30 kujaza na kupakia nyaraka zinazohusu madaraja kwenye mfumo.

“Katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais Mhe. Dkt. Samia kumekuwepo na ongezeko na uboreshaji wa masuala yanayohusu maendeleo ya walimu husasani katika ajira, upandishaji vyeo na kubadilishwa vyeo. Katika kufanya hivyo, maslahi na stahiki za walimu zimeguswa na kupewa kipaumbele kwa kiasi kikubwa” alisema.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Manyoni imeendelea kuwafikia walimu katika ziara shuleni kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi

wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

“Tumefanikiwa kuwa na ziara katika shule zilizopo katika Kata 32 za Wilaya ya Manyoni ambapo walimu 1,034 wamefikwa na elimu juu ya mambo yanayohusu maadili na nidhamu na kuweza kugawa jumla ya vitabu 119 vinavyotoa ufafanuzi wa Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Walimu.

Aliendelea kuelezea kuwa, pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

“Katika kipindi cha miaka mitatu, mashauri ya nidhamu 8 yalifunguliwa ambapo kati ya hayo mashauri matano (5) yalikusishwa na utoro, mawili (2) kukataa uhamisho na mmoja (1) kwa kughushi nyaraka,” alisema Kaimu Katibu Msaidizi huyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Manyoni ina jumla Halmashauri mbili (2) ambazo ni Manyoni na Itigi na inahudumia jumla ya walimu 1,686 wa shule za Msingi na Sekondari.

KONGAMANO LA ELIMU LAENDELEA IKIWA NI SEHEMU YA MAONESHU YA ELIMU, UJUZI NA UBUNIFU

Na Mwandishi Wetu – Tanga.

Maonesho ya Kitaifa ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika Viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal, jijini Tanga, kuanzia tarehe 25 hadi 31 Mei, 2024 yalikuwenda sambamba na kongamano la elimu lililowakutanisha wataalamu mbalimbali katika sekta ya elimu kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujadiliana mikakati ya kuendeleza Sekta hiyo.

Kongamano hilo lilifanyika katika Hoteli ya Tanga Beach Resort ambapo mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwemo Ushirikishwaji wa Watu wenye Mahitaji Maalumu katika Ubunifu na Matumizi ya Teknolojia; Matumizi ya Ujuzi na Teknolojia za Kisasa katika



Mmoja wa wasilishaji wa Mada Katika Kongamano la Elimu lililofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Tanga Beach Resort jijini Tanga akiwasilisha mada tarehe 29 Mei 2024.

Kukuza Uchumi wa Taifa; Mazingira Wezeshi ya Kujifunzia; pamoja na Mfumo wa Elimu unaoendana na Soko la Ajira.

Washiriki wa Maonesho hayo kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa washiriki waliohudhuria Kongamano hilo.



Washiriki mbalimbali waliohudhuria Kongamano la Elimu katika Hoteli ya Tanga Beach Resort tarehe 29 Mei, 2024.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWAGUSA WALIMU 973 WILAYA YA IRAMBA KWA KUWAPANDISHA VYEO

Na Mwandishi wetu – Iramba.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan walimu 973 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Iramba wamepandishwa vyeo ikiwa ni moja ya jitihada za Serikali za kushughulikia maslahi ya walimu.

Hayo yameelezwa na Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Iramba, Bw. Cosmas Z. Cosmas alipotembelewa na maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa TSC hivi Karibuni kwa lengo la kupata taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume katika ofisi hiyo.

Bw. Cosmas alieleza kuwa hatua alizochukua Rais Samia katika kulinda maslahi ya walimu, kwa upande wa Iramba zimesaidia walimu kuongeza kasi ya utendaji kazi shuleni na hivyo kuwezesha wanafunzi kufanya vizuri katika masomo yao.

“Rais Samia ameweka historia ya pekee katika wilaya yetu kwa kuhakikisha haki na maslahi ya walimu yanalindwa kwa nguvu zote. Tukiangalia mwaka 2020/2021 tulipandisha vyeo walimu 376, mwaka 2021/2022 tulipandisha walimu 70 na mwaka 2022/2023 tumepandisha vyeo walimu 527, hii ni hatua kubwa katika kuimarisha Sekta ya Elimu,” alisema.

Alifafanua dhamana ya kupandisha vyeo walimu ipo mikononi mwa Kamati ya TSC Wilaya kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015 huku akibainisha kuwa kwa upande wa Iramba kamati hiyo ilihakikisha kuwa kila mwalimu aliyekuwa na sifa ya kupanda cheo kwa mujibu wa miongozo iliyotolewa alipata haki hiyo.

Aidha, Cosmas aliendelea kueleza kuwa, katika miaka mitatu



Afisa Ajira wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Iramba, Bw. Cosmas Z. Cosmas akielezea mafanikio na hali ya nidhamu kwa walimu wa Wilaya hiyo akiwa ofisini kwake Iramba hivi karibuni.

ya Rais Mhe. Dkt. Samia, jumla ya walimu wapya 209 wameajiriwa ambao mwaka 2021 walijajiriwa walimu 52, mwaka 2022 walijajiriwa walimu 75 na mwaka 2023 walijajiriwa 82.

Alisema jambo jingine ambalo Serikali ya Awamu ya Sita imewasaidia TSC Wilaya ya Iramba ni pamoja na kuwapatia vifaa vya ofisi (kwa mfano) na usafiri wa pikipiki ambao umewawekea mazingira mazuri ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Bw. Cosmas alisema kuwa kuanzishwa kwa TSCMIC kumeleta ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Tume kuanzia ngazi ya Wilaya hadi Makao Makuu kwani umesaidia kutatua changamoto za walimu ambapo sasa hawalazimiki kusafiri bali wanaweza kutumia Kompyuta zao na hivyo viongozi wa juu kuziona kwa haraka na kuzifanyia kazi.

Akizungumzia suala la maadili na nidhamu kwa walimu, Bw. Cosmas alisema Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Iramba

imeendelea kuwafikia walimu kwa lengo la kuwaelimisha umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na Taratibu za Utumishi wa Walimu na zile za Utumishi wa Umma ili kujiepusha na kukiuka maadili ya kazi hiyo.

Aliendelea kusema pamoja na jitihada hizo wapo baadhi ya walimu wachache ambao mienendo yao ilikuwa kinyume na maadili ya kazi ya ualimu jambo lililosababisha kuchukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu.

“Katika kipindi cha miaka mitatu, mashauri ya nidhamu 13 yalifunguliwa ambapo makosa 10 yalihusu utoro, ukiukaji wa maadili ya ualimu, ubadhilifu wa mali na matumizi ya cheti kisichokuwa cha kwake. walimu 4 waliopatikana na hatia na kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi. Walimu wawili (2) walipewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 za mashahara kwa miaka mitatu waliobaki hawakukutwa na hatia” alisema Afisa Ajira huyo.

MWL. PAULINA: MADAI YA WALIMU KUWA HISTORIA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama amesema siku sio nyingi madai ya walimu yatakuwa historia kwa kuwa Serikali imeshajipanga kuyashughulikia.

Ametoa kauli hiyo wakati mkutano wake na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba na Kondoa tarehe 30 Mei, 2024 kwenye Ukumbi wa Chuo cha Ualimu cha Bustani.

Alisema kuwa hatua inayofuatia sasa ni Viongozi na Watendaji kutekeleza agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan la kubainisha changamoto zote za walimu ili zipatiwe ufumbuzi.

Mwl. Paulina alisema kuwa agizo hilo limetekelezwa kwa kuundwa kikosi kazi cha kupitia taarifa za walimu wote nchini ambapo kilibainisha changamoto sita zinazowakabili walimu.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akisaina kitabu cha wageni katika Chuo cha Ualimu cha Bustani kilichopo wilayani Kondoa kabla hajazungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Mpwapwa na Chemba leo tarehe 30 Mei, 2024.

“Changamoto hizo ni kutopandishwa madaraja kwa wakati, kubadilishwa muundo baada ya kutoka masomoni, kuchelewa kulipwa mapunjo ya mshahara baada ya kupandishwa vyeo (arrears), kutolipwa fedha za likizo kwa wakati, kutolipwa fedha za uhamisho kwa wakati na baadhi ya viongozi kuwajibu kwa lugha zinazowakatisha tamaa walimu,”

alisema Nkwama.

Alisema kuwa baada ya kikosi kazi hicho kukamilisha zoezi hilo ilibainika kuwa walimu 54,000 walicheleweshwa kupandishwa madaraja.

Mwl. Paulina alisema kuwa baada ya kubainika kwa taarifa hiyo, Serikali ya Awamu ya Sita imekusudia mwaka ujao wa fedha mara baada ya taratibu za kiutumishi kukamilika kupandisha kwa njia ya mserereko walimu hao 54,000 na wengine 52,000 watapandishwa kwa njia ya kawaida baada ya kukidhi vigezo kwa mujibu wa taratibu.

Alisema kuwa nia ya Serikali ni kuondoa changamoto zinazowakabili walimu ili wao wabaki na jukumu la kutoa ujuzi na malezi kwa wanafunzi kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Mwl. Paulina alisema kuwa kwa juhudi hizo Rais Samia amejipambanua jinsi ambavyo ameweka mazingira mazuri ya walimu kutoa elimu na uboreshaji wa elimu nchini.

Katibu huyo wa Tume ya Utumishi wa Walimu amehitimisha ziara ya kikazi kwa Mkoa wa Dodoma ikiwa ni sehemu ya kuwapongeza Walimu kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya katika kufundisha wanafunzi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akivishwa Skafu na Skauti wa Shule ya Msingi ya Mpalagwi wilayani Kondoa kabla hajaanza mkutano na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Chemba na Kondoa leo tarehe 30 Mei, 2024.

MWL. PAULINA: MADAI YA WALIMU KUWA HISTORIA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mw. Paulina Nkwama (kushoto) akisalimiana na viongozi wa Wilaya ya Chemba na Kondoa leo tarehe 30 Mei, 2024 kabla ya mkutano na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya hizo.



Baadhi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya ya Chemba na Kondoa Wakiimba wimbo wa Taifa na ule wa Mkoa wa Dodoma Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mw. Paulina Nkwama (kushoto) akisalimiana na viongozi wa Wilaya ya Chemba na Kondoa leo tarehe 30 Mei, 2024 kabla ya mkutano na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya hizo.



kabla ya mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mw. Paulina Nkwama(hayupo katika picha) leo tarehe 30 Mei, 2024.



Baadhi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari za Wilaya ya Chemba na Kondoa Wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mw. Paulina Nkwama(hayupo katika picha) leo tarehe 30 Mei, 2024 kwenye mkutano maalumu wa kupewa mbinu za kuboresha elimu na kuelezea jinsi changamoto zao zilivyoshughulikiwa na Serikali.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mw. Paulina Nkwama(katikati) akiwaongoza viongozi wa Wilaya za Chemba na Kondoa kuimba wimbo wa Taifa kabla hajaanza kuzungumza na walimu wa shule za Msingi na Sekondari wa Chemba na Kondoa leo tarehe 30 Mei, 2024.

WATUMISHI 46 WA TSC WAOMBA KUJIUNGA NA TUGHE

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Jumla ya Watumishi 46 wametuma maombi ya kujiunga na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) katika Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

Kauli hiyo imetolewa tarehe 23 Mei, 2024 jijini Dodoma na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la TSC Bw. Francis Gwankisa wakati akitoa mada kwenye mkutano wa siku moja wa Watumishi wa TSC nchini uliofanyika kwa njia ya mtandao.

Alisema kuwa ongezeko hilo limeiwezesha TSC kufikisha wanachama wa TUGHE 55 baada ya wale tisa (9) waliokuwepo hapo awali.

Bw. Gwankisa alisema watumishi wote wa TSC wakiwemo wale ambao ni waalimu waliokuwa wanachama wa vyama vingine, kwa sasa wanapaswa kujiunga na TUGHE kwa kuwa ndio Chama cha Wafanyakazi kinachosimamia wafanyakazi katika Taasisi hiyo.

Aidha, Mwenyekiti huyo wa



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Francis Gwankisa (katikati) akitoa mada kuhusu utaratibu wa kujiunga na TUGHE kwenye mkutano wa siku moja wa Watumishi wa TSC nchini uliofanyika kwa njia ya mtandao. Wengine katika picha ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC Bw. Ramadhan Ngaegela na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC Mwalimu Fatuma Muya.

TUGHE Tawi la TSC alitoa wito kwa watumishi wengine kuendelea kujiunga na Chama hicho kwa kujaza fomu na kuziwasilisha kwa viongozi wa TUGHE Tawi la TSC ili hatua za usajili wao zikamilishwe.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama ameupongeza uongozi wa TUGHE Tawi kwa

kufanikisha kuongeza idadi ya wanachama kutoka 9 hadi 55.

Alisema juhudi hizo zimesaidia kuepusha hatari ya kufungwa kwa Tawi la TUGHE la TSC ambapo ingesababisha kutofanyika kwa vikao vya Baraza la Wafanyakazi kwa kuwa ili mkutano ufanyike Tawi linapaswa kuwa na wanachama wasiopungua 10.



Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) Tawi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Bw. Francis Gwankisa (katikati) akionyesha machapisho mbalimbali ambayo yanapaswa kutumiwa na watumishi wa TSC wakati alipokurwa akitoa mada kuhusu utaratibu wa kujiunga na TUGHE kwenye mkutano wa siku moja wa Watumishi wa TSC nchini uliofanyika kwa njia ya mtandao. Wengine katika picha ni Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la TSC, Bw. Ramadhan Ngaegela na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu ya TSC, Mwl. Fatuma Muya.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania

 [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)